## Bibilia Ya Sema Nini Kuhusu Ulevi

Bibilia yalinganisha ulevi na upumbavu (Mithali 26:9) na inapeyana onyo hili: Ole wao wale waamkao asubuhi na mapema wakikimbilia kunywa vileo, wale wakawiao sana mpaka usiku, mpaka wamewaka kwa mvinyo. (Isaya 5:11). Ole wake yeye ambaye jirani yake kileo, akiimimina kutoka kwenye kiriba cha mvinyo mpaka wamelewa, ili apate kutazama miili yao iliyo uchi. (Habakkuk 2:15).Ole wao walio mashujaa kwa kunywa mvinyo nao walio hodari katika kuchanganya vileo, (Isaya 5:22). Amkeni, enyi walevi, mlie!
Pigeni yowe enyi wanywaji wote wa mvinyo, (Joel 1:5).

## Hapana Walevi Mbinguni

Mtume Paulo aliwaonya watu ya kuwa hakuna mlevi atakaeingia katika ufalme wa mungu (1 Wakoritho 6:10). Ulevi ni kitendo cha kawaida cha utu alisi wa dhambi hakuna awayeyeyote aishie katika njinsi hii atakae urithi ufalme wa mungu (Wagalatia 5:19-21).

Yesu alitoa mfano wa mtumishi muovu aliyeanza kula na kunywa na walevi, bali bwana wake atakapo rudi atamukatakata vipande na kumuweka pamoja na wanafiki, pahali pa kilio na kusaga meno (Matayo 24:48-51). Tahadhari hii kuu ni ya kuwaonya walevi wasiingie katika moto wa jehanamu, maana ulevi ni aina moja ya ukafiri (1 Wakorintho 6).

## Sumu ya Ibilisi

Ni nani mwenye ole? Ni nani mwenye huzuni? Ni nani mwenye ugomvi? Ni nani mwenye malalamiko? Ni nani aliye na majeraha yasiyo na sababu? Ni nani mwenye macho mekundu? Ni hao wakaao sana kwenye mvinyo, hao waendao kuonja mabakuli ya mvinyo uliochanganywa. Usiukodolee macho mvinyo wakati ukiwa mwekundu, wakati unapometameta kwenye bilauri, wakati ushukapo taratibu! Mwisho huuma kama nyoka na kutia sumu yake kama nyoka mwenye sumu. (Mithali 23:29-32). Ibilisi washiriwa kama nyoka na ndiposa nimeitaja ulevi kama sumu ya ibilisi.

## Chagua marafiki kwa busara

Mvinyo ni mdhihaki na kileo ni mgomvi, ye yote apotoshwaye navyo hana hekima.(Mithali 20:1)Tumetahatharishwa kutounganika pamoja na wanywao vileo mno (Mithali 23:20). Mtume petero atuonya tuepukane na wao waishio katika tamaa za mwili, living in debauchery, kuishi katika tamaa za mwili na ulevi maana watatoa hesabu ya matendo yao kwa yeye ahukumuye walio hai na walio wafu (1 Petero 4:2-5).

## Furaha Ya Ukweli

Usidanganywe Mungu hafanyiwi dhihaka. Mwanadamu huvuna kile apandacho. Yule apandaye mbegu zake katika hali ya utendaji dhambi, hivyo basi huvuna uaribifu. Na Yule apandaye kumfurahisha roho mtakatifu, huvuna uzima wa milele (wagalatia 6: 7-8) Matunda ya roho mtakatifu ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, imani, utilifu na kiasi.
Furaha ya ukweli hupatikana katika njia zilizo safi, njia zisizo za mauti.

## Kujitenga Kabisa

Mungu anatuamuru kuwa tusiwe walevi (Waefeso 5:18) Kwa wakati pia Mungu atuamuru tukane kabisa vinywaji vizito. Kama ilivyo kwa wachungaji (mambo ya walawi 10:9) Sheria za wanazareti (hesabu 6:3) Hekima ya waongozao (mithali 3:4) Nabii Danieli (Daniel 1:8) Yohana mbatizaji (Luka 1:15) Waumini wote katika hali tofauti tofauti (Warumi 14:21)

## Njia Ya Wokovu

Yesu Kristo alikuwa rafiki wa watenda dhambi na hiyo ndiyo sababu ya wasaliti wa dini walimshitu kuwa mlafi mlefi, rafiki ya watoza ushuru, na wenye dhambi

(Matayo 11:19) Yesu alikaa kwa muda na watenda dhambi ilihali yeye hakuwa mtenda dhambi. Kristo ni mtakatifu ametengwa na dhambi, ameinuliwa juu ya mawingu, msafi mwenye roho, bila malalamishi. Alijaribiwa kwa njia nyingi ilihali hakuwa na dhambi (Wahebrania 4:15) Alipenda utakatifu na akachukua maovu (Wahebrania 1:9)

Yesu alichukia dhambi lakini alipenda watenda dhambi. Hii ndiyo dhairi kwamba hakuaibika kujitambulisha na makahaba, watu waliotengwa na jamii, na wale wasiojiweza. Hii ndiyo sababu yeye alikuja katika ulimwengu huu "Sikuja kuwaita wasafi wa mioyo, bali watenda dhambi waokolewe(Matayo 9:13) Yesu alikuja kuyabadilisha maisha ya wanadamu. Anawaita walevi watubu na anawatafuta ili awaokoe.

Yesu alikuja toka binguni yeye yuna Mungu ilihali alijifanya mwanadamu ili atuonyeshe njia na atuondolee dhambi, ambayo ni kifo. Yesu akiwa msalabani, alimwaga damu yake ili asafishe dhambi zetu. Yesu alikuja kwa ajili yetu, na alifufuka siku ya tatu ili kumwaibisha shetani na kutupa zawadi ya uzima wa milele kwa Yule anayeamini.

Kama umekuwa mlevi fungua moyo wako kwa Mungu mfalme kisha uombe ombi hili " Mfalme wa mbingu na nchi naja mbele yako kwa jina la Yesu kristo. Natubu dhambi zangu. Nakiri kwamba nimekosa mbele yako na nimeharibu maisha kwa ajili ya pombe Naomba unisamehe na unisafishe. Namchukua Yesu kama mfalme na mkombozi kwa njia ya imani kupitia kwa damu yake. Nguvu za dhambi zimevunjwa . Nakuhitaji kwa ukombozi. Nakemea roho wa ulevi na kuzivunja nguvu za kishetani, huku nikijuwa kwamba neno la Mungu lasema "Jisalimishe kwa Mungu. Mkatae shetani na atakutoroka (Yakobo4:7) Asante kwa kunipa ukombozi na neno lako lihimidiwe milele na milele. Amina."

Kwa sababu umekuwa mkristo, umezaliwa tena kupitia kwa roho mtakatifu, yafaa ukomae katika uhusiano wako na Mungu.

Yafaa ujifunze kuisikia sauti ya Mungu na ufuate njia zake:

1). Soma Biblia
2). Omba na uongee na Mungu moyoni mwako
3). Batizwa na ujiunge na Kanisa linalompendaza Yesu kristo.

Kwa maelezo zaidi, *tupate kwa tuvuti yetu:*

***Pastor David (Okame)* 0702296772**

**www.evangelistmatthew.com**

# NA UPUMBAVU WA ULEVI

KULINGANA NA HEKIMA YA

# KUMFUATA MUNGU

**WAFANYA NINI NA MAISHA YAKO?**